

Muht Na. 57/2017-KUJADILI TAARIFA ZA WENYEVITI WA KAMATI

Taarifa za wenyeviti wa kamati ziliwasilishwa na wenyeviti wa kila kamati kama ifuatavyo;

KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII

Iliwasilishwa taarifa kuwa kamati ilifanya kikao chake cha robo ya nne tarehe 29.08.2017 kamati ilijadiliana taarifa za utekelezaji wa kila idara inayoundwa kamati hii na baada ya majadiliano hayo kamati imeshauri na kuazimia yafuatayo

- Katika maeneo ambayo kuna upungufu mkubwa wa madawati ufanyike utaratibu wa kupeleka madawati kutoka maeneo yenye zidio la madawati na michango ya harambee ya madawati iendele kufuatiliwa ili madawati yatengenezwe na kupelekwa maeneo yenye upungufu.
- Ilikuweza kudhubiti mapato na matumizi ya fedha za CHF, taarifa za mfuko ziwe zinawasilishwa katika mikutano ya vijiji, WDC, na Halmashauri na Maafisa waandikishaji wapewe maelekezo haya.
- Kamati pia ilipitisha maombi ya kufunguliwa kwa duka la dawa ndani ya hospitali ili wananchi waweze kupata dawa kwa urahisi.
- Kamati pia imepitisha mapendekezo ya Bodi ya Afya ya kuwataka wasio wajawazito wa watoto kuchangia gharama za mafuta katika magari ya kubebea wagonjwa aidha walishauri kuwa umbali na kiasi cha mafuta kitakachotumika viainishwe na kubandikwaaaa katika vituo vya kutolea huduma za afya ili wachangiaji waweze kujua.
- Kamati iliagiza wataalaamu kwenda kutafuta mgogoro Iwondo ambako kuna mgogoro wa chombo huru cha watumia maji.

Baraza lilipokea taarifa iliyowasilishwa na kisha kuipitisha.

KAMATI YA HUDUMA ZA UCHUMI

Iliwasilishwa taarifa kuwa kamati ilifanya kikao chake cha robo ya nne 2016/2017 mnamo tarehe 29.08.2017 na kisha kushauri na kuazimia yafutayo;

- Wananchi ambao wanamiliki maeneo makubwa ya ardhi ufanyike upimaji shirikishi wa viwanja. Kuandaliwe andiko juu ya upimaji huo na kisha uwasilishwe katika kikao kijacho.
- Msukumo wa ulipaji fidia wa viwanja vilivyonunuliwa ufanyike kwa wanachi wote walionunua viwanja hivyo na si kwa Wah. Madiwani pekeyake. Dhumuni hasa ni kuwawezesha walionunua viwanja hivyo kuweza kuviendeleza.
- Wahusika waliofilisi SACCOS wafuatiliwe ili kuweza kurudisha fedha wanazodaiwa, kwa kutoa taarifa juu ya idadi ya majina ya wanaodaiwa na kile wanachodaiwa vilevile taratibu za kisheria zifuatwe juu ya watu hao waliofilisi.
- Gari la kuzoa taka lishughulikiwe/litengenezwe kwa haraka ili kuweza kuzoa taka sehemu za mjini.

Baraza lilipokea taarifa iliyowasilishwa na kisha kuipitisha.

KAMATI YA UKIMWI

Iliwasilishwa taarifa kuwa kamati ilifanya kikao chake cha kawaida Robo ya nne mwaka wa fedha 2016/2017 mnamo tarehe 29/08/2017. Katika majadiliano wajumbe walitoa mapendekezo, maazimio na ushauri ufuatao;

- Kutokana umuhimu wa wahudumu wa nyumbani, na kwakuwa wahudumu hao hawapewi posho mara baada ya mfadhili TUNAJALI kumaliza mradi , kamati ilishauri menejimenti ione namna ya kuwezesha posho ili wahudumu hao waweze kufanya kazi kwa moyo na kuwajibika ipasavyo.
- Kamati ilitoa wito kwa idara mbali mbali kushirikiana ili shughuli zilizopangwa kutekelezwa zitekelezwe kwakuwa Serikali haikutoa pesa .
- Kamati ilitaka suala la usugu wa dawa unaojitokeza kwa watu waliotumia dawa za ARVs kwa zaidi ya miaka 5

Baraza lilipokea taarifa iliyowasilishwa na kisha kuipitisha.